MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 1 TOLEO 1

AUGUSTI 19, 2008

KIJARIDA CHA BURE

VIGOGO WA EPA KUKWEPA ADHABU?

Majengo ya Benki Kuu

Na. Fred Katunzi

Mmoja wa watu ambao makampuni yao ya kubadilisha fedha yalihusishwa na fedha za EPA ameiambia CHECHE kuwa kuna kila dalili kuwa kuna kila dalili kuwa vigogo waliosuka na kufanikisha wizi wa EPA wakasalimika katika adhabu na watu wa kati ndiyo watakaobebeshwa mzigo huo

"waliobuni wizi huo na kuufanikisha watasalimika na sisi wengine ambao tuliponzwa na tamaa zetu kuwasaidia ndio tutakaojikuta tunabebeshwa mzigo huo" alisema mmiliki huyo kwa lafudhi yake kali iliyoashiria kuwa ni mtu aliyekulia maeno ya mwambao wa Bahari ya Hindi akizungumza kwa simu na Cheche. Mmiliki huyo alielezea jinsi gani walijikuta wanaingizwa kwenye mtego huo mchafu kwa sababu ya tamaa yao ya fedha.

> Tulichowafanyia Watanzania ni aibu na sisi sote tunastahili adhabu,

" nilifuatwa na dereva wa mtu mkubwa tu ambaye amekuwa akileta fedha hapa kubadilisha" Alisema mmiliki huyo akitaja jina la kampuni yake ya kubadilishia fedha iliyoko Jijini Dar. "Huyo bwana ndio alikuwa akitumwa mara nyingi na Afisa mmoja wa serikali mwenye cheo cha juu kubadilisha fedha, Tulikuwa tukimfahamu vizuri tu" Aliendelea.

Kwa mujibu wa siku mmiliki huyo na habari moja dereva huyo alikuja kuna kiasi kikubwa cha fedha ambacho bosi wake alikuwa anataka kubadilisha kwa haraka na tena bila kufuata taratibu za Kibenki kama inavyotakiwa kisheria. Mmiliki huyo anasema kuwa alimhakikishia dereva huyo kuwa hilo si tatizo kwani tayari walishakuwa na vitabu vya aina mbili – vile vinavyobeba taarifa za kupelekwa Benki Kuu na vile vya geresha.

"Tukamkubalia hasa alipotaja kiasi chenyewe" alisema mmiliki huyo akijiamini lakini

Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja**
- **UKIMALIZA KUSOMA MPE MWINGINE**

HOJA YA MWANAKIJIJI— UFISADI NI VITENDO!

Je waweza kujua kuwa mtu ni fisadi kwa kuangalia gari analoendesha, cheo alichonacho au nyumba anayoishi?

Je, fisadi anaweza kujulikana kwa kuangalia elimu aliyonayo, mavazi, rangi, au kabila lake?

Haiwezekani! Ufisadi ni vitendo. Mtu ambaye anatabia na maisha ya kifisadi anatambulika kwa vitendo vyake.

Mtu ambaye anatumia fedha za umma vibaya na kwa manufaa yake, ambaye anatumia madaraka yake kujinufaisha yeye mwenyewe na kuwakandamiza wengine, mtu huyo ni fisadi.

Fisadi basi hawezi kujulikana kwa kuangalia vitu vya nje nje isipokuwa vitendo vyake vitamuumbua.

Hivyo utaona fisadi siyo lazima awe mwanasiasa; anaweza kuwa mwalimu, mchungaji, padri, shehe, meneja, na hata tarishi!!

Kwa sababu ufisadi ni vitendo; anayefanya ufisadi, yeye **FISADI!**

Ndani ya Toleo Hili

Watakwepa adhabu?	1
Ufisadi ni vitendo	1
Kashfa Tume ya Maadili	2
Wanafunzi watoa somo	3
Ufisadi wa Ngono	3
Vikatuni na Picha	4
Kutoka JamiiForums	4

HABARI MBALIMBALI

TUME YA MAADILI YAKABALIWA NA KASHFA

Na. Mahmoud Rashid

Tume ya Maadili ya viongozi yenye makazi yake Jijini Dar-es-Salaam inanyemelewa na kashfa kubwa ya ubadhirifu na ukosefu wa maadili baada ya wanaojiita wafanyakazi wa tume hiyo kuandika na kusambaza nyaraka mbili zinazoelezea kile wanachodai kuwa ni uongozi mbovu wa Mwenyekiti wa tume hiyo Jaji Stephen Ihema.

Katika barua yao ya kwanza iliyoandikwa tarehe 10 Julai, 2008 kwenda kwa Katibu Mkuu kiongozi Bw. Philemon Luhanjo wafanyakazi hao wanadai kuwa Jaji Ihema na watumishi wengine wa ngazi za juu wa tume hiyo " wamekuwa wakicheza na Bajeti ya Sekretarieti wapendavyo, huku wakikandamiza haki za wafanyakazi kwa kiwango cha hali ya juu, kuwanyima posho stahili za watumishi, wanaposafiri, kupunja stahili nyingine, lakini kwa kuwa ni wao tu ndio wanaoijua bajeti ya Sekretarieti inasemaje,wameweza kupata hati safi toka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kwa kufoji baadhi ya malipo na kusingizia mambo fulani yametumika kwa ajili ya watumishi, ilihali wafanyakazi hawajui na wala hawakupewa hayo mambo"

Mama huyu ni jasiri ameshamfungulia Ihema mashtaka kwenye mahakama ya kazi!

Katika madai mengine yaliyoandikwa katika waraka huo wa kwanza wafanyakazi hao wanadai kuwa " Sekretarieti ina madeni lukuki yakiwemo ya Uzinduzi wa FEAT,huduma nyingine zilizotolewa na wadau mbalimbali kwa Idara hii, Ofisi za Kanda ndo zina hali mbaya hadi kufikia kukopa Huduma za maji, Umeme, matengenezo ya magari na vifaa vingine."

Kuhusu uongozi wa Kamishna wa Maadili, barua hiyo inadai kuwa Jaji Ihema amekuwa akiiongoza taasisi hiyo nyeti kwa utawala wa kiimla. Barua hiyo inadai kuwa ".. mmoja wa wahanga wa chuki yake ni Magreth Kimambo aliyekuwa Meneja Mradi wa Mfuko wa Uadilifu,Uwazi na Uwajibikaji ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia, alimnyanyasa mno kwa maneno ya dharau kama vile mwandiko wake ni kama wa Bata, na kusitisha ajira yake kinyemela, bila kuzingatia Kanuni za Utumishi wa Umma zinazosema mtu aliye kwenye mkataba hana Probation Period, lakini kwa busara zake Ihema alilazimisha kuwe na kipindi cha uangalizi kwa mama huyu, lakini kwa kuwa mama huyu ni jasiri, ameshamfungulia mashtaka Ihema katika Mahakama ya Kazi akidai kulipwa stahili zake zote."

Katika barua yao nyingine yenye kuonesha imeandikwa siku mbili kabla ya hiyo nyingine wafanyakazi hao walidai wanataka Jaji Ihema aondolewe kwenye wadhifa wake wa Kamishna wa Maadili. Watumishi hao wanatoa sababu kumi na moja za kwanini Jaji Ihema hafai kushika nafasi hiyo.

Tume ya Maadili ndicho chombo cha Kikatiba kilichoundwa kusimamia maadili ya viongozi wa umma kuanzia Rais mwenyewe na kinaongozwa na Kamishna.

Barua hizo za tuhuma nzito zinapatikana kwenye tovuti yetu ya http://www.klhnews.com

KAFARA YA EPA (kutoka Uk 1.)

akionesha hisia ya kutambua kosa lake. "Baada siku chache walitupigia simu kuwa fedha ziko njiani na walipofika tuliingia nao ofisini na kufanya mabadilishano kutoka dola kwenda fedha ya Kitanzania kwa kiwango tofauti na cha kawaida. Mabadilishano hayo hayakuingizwa kwenye vitabu vya taarifa za Benki Kuu tunazotakiwa kuwa nazo"

Kama wangeenda mahakamani ..vigogo wangetajwa hadharani!

Mmiliki huyo anasema kuwa siyo yeye tu bali wafanyabiasharra wengine walihusishwa katika kubadilisha fedha hizo baada ya kufuatwa na viongozi na watendaji mbalimbali wa serikali na viongozi wa CCM. Anachosema ni kuwa tatizo kubwa ni kwamba wale vigogo wenyewe hawakutaka kufanya mambo moja kwa moja wao wenyewe. "Tunawajua kwa majina, na madereva au wale madalali wao wanawajua kwa majina" alisema mmiliki huyo. Walitumia watu wa kati na wao wenyewe walipopewa hiyo fedha wakaiingiza katika miradi mbalimbali ikiwemo miradi ya majengo, maofisi au kuanzisha makampuni wakiwa na mtaji mkubwa tu. Sisi tuliambulia kamisheni nzuri tu.

Alipoulizwa kama atakapoadhibiwa itakuwa ni kuonewa mmiliki huyo alisema kuwa walifanya makosa na adhabu watakayopewa ni sawa kwani wameponzwa na tamaa zao. "Hata hivyo, kama wangeenda Mahakamani kina Mwanyika basi vigogo wangetajwa mbele ya kiapo lakini hawakuwa na mpango huo na wameamua kumalizana chini kwa chini. "Tulichowafanyia Watanzania ni aibu na sisi sote tunastahili adhabu, asionewe mtu au kupendelewa" alisema.

Wizi wa fedha za EPA ulitokea kati ya mwaka 2005/2006. Mapema mwaka huu Rais Kikwete aliunde timu kuwachukulia hatua wahalifu wa EPA. Hata hivyo tume hiyo inadaiwa kuandaa ripoti badala ya kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wahusika kama ilivyoagizwa na Rais.

Soma Bure
hoja zenye nguvu

NGUVU ZA HOJA

WANAFUNZI WAMETOA FUNDISHO

Na. Kevo

WATOTO wetu wamefanya kile ambacho sisi wazazi wao tumeshindwa, na badala yake tumeishia kufanya kile watoto hao wanachoweza kusema ni kukalia siasa tu.

Watoto wetu hawa wanaosoma shule za msingi na za sekondari za Dar es Salaam waliandamana siku chache zilizopita kupinga ongezeko la nauli ya mwanafunzi kutoka Shilingi 50 hadi Shilingi 100 kwa safari moja.

Wameweza kujiratibu na kuandamana siku mbili tu baada ya ongezeko hilo kutangazwa. Ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wote wa jiji la Dar es Salaam, walioandamana hawakuwa wengi lakini wamefikisha ujumbe kwa watawala.

Najiuliza mno, na kuogopa, ingekuwaje iwapo wangepata mwezi mzima wa kuji-

andaa.

Ni 'Mene mene tekeli na peresi', maandishi ukutani ambayo kwa hakika watawala wetu wanapaswa kuyasoma na kuyatafutia ufumbuzi haraka iwezekanavyo.

Walichothubutu kufanya watoto wetu ni ushahidi kamili na wa wazi kabisa kwamba hiki ni kizazi ambacho hakitakuwa na ukondoo uliowakuta wazazi wao uliobatizwa jina refu la 'amani, uvumilivu na mshikamano wetu'.

Kuna somo hapa. Watoto wetu wamethubutu kuandamana wakati walimu wao wameipa serikali siku sitini kukamilisha madai yao ama sivyo wataitisha mgomo wa walimu nchi nzima. Tumeambiwa kuwa wanajazishana fomu ili kujua idadi ya watakaokuwa tayari kujiunga na mgomo.

Hii sio mara ya kwanza walimu kutishia kugoma. Wameshafanya hivyo mara nyingi tu huko nyuma; lakini kila mara maneno mazuri ya viongozi wa Serikali yameweza kuwashawishi 'warudishe majeshi nyuma'.

Watoto wetu wameandamana kuonyesha kutokubaliana kwao na nauli mpya waliyotangaziwa. Wamepigana vita inayopaswa kuwa ya wazazi wao. Ni bahati mbaya tu kwamba wamepata jibu lile lile ambalo wazazi wao walio wafanyakazi na kaka na dada zao wa vyuo vya elimu ya juu wamekuwa wakipewa na watawala kila walipotishia kugoma ama kuandamana.

Tusifike huko. Ni vyema watawala wakasoma alama za nyakati 'zinazoandikwa' na watoto wa shule na wananchi wengine wa kada mbalimbali na kufanya kile jamii inachotegemea kutoka kwao badala ya visingizio hafifu vya 'kuna watu wanawatumia'

Ufisadi wa ngono ni ufisadi

Na. Jessica Leonard Fundi

Kama kweli tunataka kupigana na ufisadi nchini tusichague uwanja mmoja bali tupigane nao katika viwanja vyote na mahali popote utakapojitokeza. Eneo ambalo nalipendekeza leo ni eneo lnalohusiana na ufisadi wa ngono katika maofisi ya serikali, binafsi, na taasisi mbalimbali za umma na hata kwenye asasi za kijamii.

Sheria ya Makosa ya Ngono ya mwaka 1998 iliyofanyia mabadiliko pia sheria ya Kanuni za Adhabu inaeleza wazi kuwa kuna makosa ya udhlilishaji wa kijinsia ambayo yanaweza kufanyika katika maofisi au sehemu mbalimbali.

Tatizo kubwa la sheria hiyo ni kutokataza mahusiano ya kingono kati ya mtu mwenye madaraka na aliye chini yake na endapo kunatokea kitu kama hicho ni ni bosi ndiye anayeadhibiwa.. Na anapohama hapandishwi cheo anabakia hapo au anateremshwa.

Mara nyingi kina dada wamekuwa wakidhalilisha kijinsia ili kukubali mahusiano ya kingono na wakubwa wao wa kazi ili kuhakikisha ajira zao zinaendelea kuwepo lakini zaidi ili wapate nafasi ya kuendelea mbele. Baadhi ya mabosi wanaume tena pasipo kificho wamekuwa wakiweka wazi kabisa kuwa ili "fulani" afanikiwe hapo kazini basi ni lazima awe tayari kufungua sketi yake.

Ni kweli wapo kina dada ambao na wao wenyewe wakijua tabia hii wamekuwa wa kwanza kuanzisha mahusiano ya namna hiyo na mabosi wao kwa kuwatumia ishara mbalimbali za kukaribisha utongozaji kutoka kwao. Ipo haja ya kufanya mabadiliko makubwa ya sheria hiyo ili kupafanya mahali pa kazi kuwa salama kwa dada, mama, na rafiki zetu.

Tutajenga mazingira ya heshima, usalama, na utu kazini. Na kwa kufanya Tukifanya hivyo tutaanza kufanya mahali pa kazi kuwa ni kweli pa kazi badala ya "pa kazi". Tutaweka mazingira ambapo mama, dada, rakifi na ndugu zetu wanaweza kufanya kazi pasipo kuhofia kudhalilishwa au kufisadiwa kingono. Tutajenga mazingira ya heshima, usalama, na utu kazini. Na kwa kufanya hivyo tutakuwa tunafanikiwa katika vita dhidi ya ufisadi.

Soma bure

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

KATUNI ZA WIKI

Picha ya Wiki

Wawakilishi wa Tanzania kwenye Mashindano ya Olimpiki huko Beijing wakipita mbele ya watazamaji siku ya ufunguzi Augusti 8, 2008



KUTOKA MTANDAO WA JAMIIFORUMS

MJADALA WA EPA

EPA ni uwizi wa wazi na Serikali haipaswi kupata kigugumizi. Maelekezo ya Rais kwa Kamati ya Mwanyika yako wazi, na hayakuhitaji Taarifa kupelekwa kwa Rais, labda Taarifa ya utekelezaji. **Dr. W. Slaa**

Kina Mwanyika na wenzake, walitakiwa, "kuchunguza na kuchukua hatua zipasazo za kisheria kwa makampuni na watu waliohusika na uhalifu huu. Rais amewataka watumie ipasavyo mamlaka na madaraka waliyo nayo kwa mujibu wa sheria." sasa wanatuambia wanasubiri kukabidhi ripoti, ni ya NINI? **Halisi**

Ama kweli haya ni mazingaombwe, Raisi kaagiza utekelezaji, wao wana andaa ripoti juu ya ripoti, ina maana wanataka raisi ndo afanye kazi ya polisi kuwakamata watuhumiwa (aka wezi?) **Rwabugiri**

Hapo ni changa la macho tu. JK na genge lake hawana nia wala mpango wa kuwachukulia hatua hao majambazi waliochota pesa zetu - **Mtanzania**

Mnajisumbua bure tu kumshambulia Mwanyika,Mwema,na Hosea. wakati huohuo mnamuonea haya na kumuogopa Raisi ambaye ana final say. – **Joka Kuu**

Kweli watanzania katika mika 10 iliyopita tumefanya kazi sana na hatujawa masikini sana wa pesa kama ulivyokuwa miaka 20 iliyopita, lakini hizo pesa zote zinaenda mikononi mwa wezi wachache ambao hata kukamatwa ni vigumu—**Bongolander**

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Ansbert Ngurumo—Makala

Jeffrey Msangi—Makala

Kwa maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com